



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA**



TAARIFA KWA UMMA

**MABADILIKO YA UKUMBI NA TAREHE YA MAHAFALI
YA 11 YA KITAALUMA KWA WAUGUZI NA WAKUNGA.**

Dodoma; 09.04.2024

Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania, anawataarifu Wahitimu wote wa kozi za Uuguzi na Ukunga waliofaulu Mtihani wa Usajili na Leseni uliofanyika tarehe **16.02.2024** kuwa, Kumekuwa na mabadiliko kidogo ya Ukumbi na Tarehe ya Mahafali ya kumi na moja ya kitaaluma ya kutunuku Vyeti vya Usajili na Leseni, ambayo kwa sasa yatafanyika siku ya Ijumaa tarehe **19.04.2024** kuanzia **Saa 01:00 Asubuhi** katika ukumbi wa **LAVANDA HALL** Jijini - Dodoma ambapo mada mbalimbali zitatolewa kisha kiapo.

Maelekezo ya kufika Ukumbini; Ukumbi upo Karibu na Ukumbi wa mikutano wa **MABEYO HALL** Jijini Dodoma.

Washiriki wote mnatakiwa kuthibitisha Ushiriki wenu kwa kujaza fomu ya Mahafali kupitia **TOVUTI** ya Baraza la Uuguzi na Ukunga www.tnmc.go.tz.

Aidha, washiriki wote mnaelekezwa kuwa, mnatakiwa kuvaa Sare ya Kitaaluma **“Professional Uniform”** iliyoidhinishwa na Baraza la Uuguzi na Ukunga kama ifuatavyo: -

1. **WANAWAKE**- Magauni au Suruali na Blauzi rangi nyeupe ndefu.
2. **WANAUME**- Kaunda suti- Shati jeupe na suruali dark blue
3. **VIATU**- Vinavyofunika miguu na siyo vya wazi, viwe vya rangi nyeusi, nyeupe au brown.
4. Kitambulisho cha NIDA, Mpiga kura, Indexing Card au cha kazi kwa wale walioajiriwa.

NB: Sandozi au Kandambili haviruhusiwi.

Kwa mawasiliano zaidi piga namba 0682896529,0622958841 na 0762003800

Imetolewa na;

**Ndimmyake Mwakapiso
Afisa Uhusiano na Mawasiliano**